

MATUMAINI PROG NO: 2520

TITLE: GOD WANTS YOU.

SUMMERY: KINAZUNGUMZIA KUHUSU VILE AMBAVYO MUNGU ANATAKA KUKULETA KWAKE.

TEXT: WAEBRANIA 12:118-24

MADA: MUNGU ANAKUTAKA.

.....

Hujambo na karibu sana kwenye fursa hii ambayo tumepewa na Mungu ili tukaweze kujifunza neno lake.

Ni tumaini langu ya kwamba ungali umelindwa vyema kabisa naye Mwenyezi Mungu. Nami kwa upande wangu niko mzima nikimshukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kushiriki Pamoja nawe.

Natuombe;

OMBI....Baba yetu uliye Mbunguni,,,tunakushukru kwa fursa hii ambayo umetupatia ili kujifunza tena kulihusu neno hili Lako kupitia kwa usaidizi wa Roho Wako.

Ni kwa Yesu tumeomba Amen

Mpendwa,,,hiki ni kipindi cha Matumaini kutoka TWR Kenya.
Kichwa cha fundisho letu la leo ni,,,,,*Mungu Anakutaka* .

Somo ni kutoka kwenye Waraka kwa Waebrania 12:18-24.

Namna ya kupatana nawe ki-mawasiliano,,nitakufahamisha pale mwishoni mwa lesson ya leo.

Pata kwanza baraka hizi kabla ya kuendelea mbele.....

WIMBO:

Ni wimbo namlilia Malebo wakiwa ni wana-Sifa Sounds wakifanya cover ya wimbo wake Mtumishi Faustine Munishi. Asanteni na Mungu Awabariki sana.....

Mimi naitwa, Vincent Amara.

Katika dunia hii,,kuna aina mbili za nguvu kubwa zinazofanya kazi hadi wa leo hii. Nguvu ya kwanza kabisa ni kutoka kwake Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, mwenye upendo na rehema nyingi. Nguvu nyingine ni ya Shetani, adui wa Mungu, ambaye kazi yake ni kuharibu, kudanganya, na kuwafanya watu watengane na Mungu.

Mpendwa,,kila kuchao,,,mwanadamu huvutwa na nguvu hizi mbili. Yaani Shetani hutafuta kuwafanya watu kuwa mateka wa dhambi, hofu, na uharibifu. Huku naye Mwenyezi Mungu, kwa rehema zake kuu, akiwa ameandaa njia ya ukombozi ili kutuweka huru.

Habari njema ni kwamba Mungu anakutaka ukaweza kuwa karibu naye. Anakutaka upokee msamaha, uzima, na zaidi sana wokovu.

Tunapozama kwenye Waraka huu kwa Waebrania 12:18-24,,,tunaenda kuona kile Mungu amefanya ili kuturejesha Kwake.

Neno kwenye Waraka huu linasomeka hivi;

18. Kwa maana hamkuufikilia mlima uwezao kuguswa, uliowaka moto, wala giza, na tufani;

19. na sauti ya tarumbeta, na sauti ya maneno; sauti ambayo wale walioisikia waliwasihi lile neno lisisemwe kwao tena;

20. (Kwa maana hawakuweza kustahimili neno lililoamriwa, Na kama mnyama akiugusa mlima, atapigwa kwa mawe, au kwa mishale;

21. Na tukio hilo lilikuwa la kutisha hata Musa akasema, Naogopa sana na kutetemeka;

22. Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na jeshi lisilohesabika la malaika;

23. Kwa mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa wote, na roho za wenye haki waliokamilishwa;

24. na Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili.

Kutokana na kifungu hiki tunajifunza namna Mungu anavyoonyesha kwamba anakutaka umkaribie. Yaani njia ambazo ni kutuleta kwake.

Njia ya kwanza kabisa ni Mungu Alijifunua kwa Nguvu Kuu.

Mwenyezi Mungu alimpa Musa ufunuo mkuu katika Mlima Sinai. Neno linatuambia kwamba,,,kulikuwa na moto, giza, tufani, sauti ya tarumbeta, na sauti ya Mungu mwenyewe.

Rafiki yangu,,hili halikuwa tukio la kawaida. Ulikuwa ufunuo wa utukufu na ukuu wa Mungu. Mlima ulikuwa umejaa uwepo wa Mungu kiasi kwamba watu waliogopa sana.

Pili ni kwamba Mungu aliweka mipaka kuzunguka mlima au ni seme kwa kizuizi cha enzi, ili kuonyesha kwamba ulikuwa mtakatifu. Hakuna mtu wala mnyama aliyetakiwa kuukaribia kwa sababu Mungu alikwa hapo.

Kwenye aya ya 21,,neno linatuelezea ya kuwa hata naye Musa mwenyewe alisema hivi; “Naogopa sana na kutetemeka.”

Kupitia kwa ufunuo huu, Mungu alikuwa anaonyesha utakatifu wake na mamlaka yake juu ya vitu vyote.

Hata wa leo hii pia,,Mungu anajifunulia kwetu kupitia kwa Neno lake,nguvu zake,kazi zake na zaidi sana kupitia kwa Mwanawe Yesu Kristo.

Mungu anapotujulisha ukweli wake, anafanya hivyo kwa sababu anatamani tumkaribie na tumjue.

Msikilizaji wangu,,Utakatifu wa Mungu Unatufundisha Haja ya Wokovu

Katika Mlima Sinai, hakuna mtu wala mnyama aliyeruhusiwa kuugusa mlima huo. Mungu aliweka mipaka kwa sababu uwepo wake ni mtakatifu sana.

Hii inatufundisha kwamba mwanadamu mwenye dhambi hawezi kuingia mbele za Mungu kwa nguvu zake mwenyewe.

Ni dhambi tu,,ndiyo hututenganisha na Mungu. Anachukia dhambi iliyo ndani ya mwanadamu,,lakini humpenda huyo mwanadamu.

Neno kwenye chuo cha Nabii Isaya 59:2 linasema;“Maovu yenu yamewatenga ninyi na Mungu wenu.”

Lakini jambo la kushangaza ni hili,,,ingawa Mungu ni mtakatifu sana, bado anatamani mwanadamu amkaribie.

Ndiyo maana alitengeneza njia ya wokovu kupitia kwa mwanawe Yesu Kristo.

Mungu hataki tuone utakatifu wake na kukata tamaa. Anataka tutambue hitaji letu la msamaha na kumrudia yeye.

Njia ya tatu na ya kumalizia kwa leo ni kwamba,,Mungu Ameandaa Mapokezi ya Ajabu kwa Waamini.

Dadangu,,,Waraka huu kwa Waebrania kwenye sura hii ya 12,,, tunaonyeshwa baraka kubwa ambazo Mungu amewaandalia wale wanaomrudia.

Biblia inasema ya kwamba tumekuja;kwenye Mlima Sayuni,katika mji wa Mungu aliye hai,Yerusalemu ya mbinguni,kwa jeshi la malaika,kwa kanisa la wazaliwa wa kwanza, kwa Mungu Mwamuzi wa wote,kwa roho za wenye haki waliokamilishwa, kwa Yesu Mpatanishi,na zaidi mno na,, kwa damu ya kunyunyizwa.

Rafiki yangu,,kunayo mapokezi ambayo ni ya ajabu sana yenye Mungu ameandaa kwa watoto wake.

Kupitia kwa Mwanawe Yesu Kristo,tunapokea msamaha,tunapatanishwa na Mungu,tunakuwa sehemu ya familia ya Mungu, na hatimae tunapokea uzima wa milele.

Damu ya Yesu inanena mema kuliko damu ya Habili kwa sababu damu ya Yesu inatuletea rehema,msamaha,na hata wokovu.

Msikilizaji wangu,,,duniani kote,,hakuna mahali pengine ambapo mwanadamu anaweza kupokea upendo mkubwa kama huu.

Kwa kumalizia,,nataka kukuhakikishia ya kwamba,,Mungu anataka sana mimi pamoja nawe tumjue vizuri,,Anakutaka uokolewe na zaidi mno Anakutaka uwe huru kutoka katika nguvu za dhambi na Shetani.

Kwa sababu hiyo,,,alijifunua kwa nguvu zake,akaonyesha utakatifu wake, na hatimae akaandaa njia ya wokovu kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

Hakuna jambo ambalo Mungu hajaweka tayari, kwa ajili ya wokovu wako rafiki yangu.Bwana na asifiwe sana.

Nataka kukuulizia swali hili ambalo ni la muhimu sana kwako. Nipatie jibu lako kupitia kwa anwani ya pale mwishoni mwa kipindi hiki.

Swali hilo ni Je, wewe,,utamwitikia?

Ndugu pamoja na dadangu,,nakusihi ya kwamba,,,usiikatae neema ya Mungu. Njoo kwake kwa imani, mpokee Yesu Kristo, na uanze maisha mapya pamoja naye.

Mungu wetu Baba wa Mbinguni anakusubiri kwa upendo mkubwa tena zaidi.

Nataka kukuacha na kifungu hiki cha kukutia Moyo kutoka kwenye Injili Yohana 6:37,,,ambapo Mungu anatuambia hivi,“Yeye ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.”

Mwiitikie maishani mwako,,nawe bila shaka utafanyika kuwa Mwanawe.

Ningependa tukahairishe kwa maombi.

Ombi.....

Uliye tukuka zaidi ya kila kitu,,Mfalme wa Wamfalme,,,kwa mara nyingine,,tunasema ni asante kwa ajili nafasi hii ya fundisho hili kuhusiana na vile Unatutaka kukurudia.Tunakuomba ukatuongoze ili tukaweze kukufikia hatimae.

Ni kwa Yesu tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu.Kipindi cha matumaini kutoka Twr.Leo ujumbe wetu umekuwa ni,,,,Mungu Anakutaka.

Tumeutoa kwenye waraka kwa Waebrania 12:18-24.

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni
mwa kipindiki hiki cha leo kwa sababu ya mawasiliano kati yetu na wewe. Kabla ya
kukusomea anwani hiyo,,.....

WIMBO.....

Na kwa kweli kabisa Damu ya Yesu inanena mema.Asane sana mtumishi Ev.
Placide kwa kazi hiyo safi ya Mungu...Ubarikiwe sana.....

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505
NAIROBI KENYA x2
Simu/Sms 0721970520 x2
Barua Pepe-barua@twr.co.ke
Kwenye Youtube ni @twrkenya

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina
langu ni Vincent Amara.....Kwaheri